## MUONGOZO WA USAHIHISHAJI

## KISWAHILI

1.

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | xi | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| C | D | A | C | A | D | A | A | A | A |

1 @ = Alama 1

2.

| i | ii | iii | iv | v | vi |
|---|---|---|---|---|---|
| G | E | F | D | A | H |

1@=Alama 1

3. (a) i) Huyu hapendi ugomvi

ii) Mafanikio alianguka wakati anakimbia

iii) Mtoto angepelekwa hospitalini mapema angepona

iv) Mzee Peko alichinja mbuzi wake wote

v) Kengele alivuka barabara nyingi kwa wakati mmoja

(b)

i) Huonesha nafsi ya pili ya mtenda wa jambo mfano
Mnaimba
Mnasali

ii) Huonesha urejeshi wa mtendwa/ Yambwa tendwa (nafsi ya pili)
Tulimzawadia Nyumba
Wamemkuta amefariki dunia

iii) Kubainisha idadi katika umoja mfano
Mtu
Mtoto

iv) Husaidia katika unominishaji wa vitenzi mfano
Cheza mchezo
Soma Msomi

v) Kubainisha uraia na utaifa

Mfano
Mtanzania
Mkenya **(Alama 9)**

4 (a) i) Huonesha  nafsi , mfano ni-nacheza
ii) Huoneesha njeo; a-na-lili-a
iii) Huonesha hali mbalimbali; anaimba-hambi-huimba
iv) Huonesha urejesshi ; a-liye-sema
v) huonesha kauli mbalimbali; soma, somea, somesha

(b) a) **Mofolojia** ni tawi la sarufi linalojishughulisha na namna au jinsi maneno yalivyonyambuliwa (upangaji wa mofimu) na kazi yake katika sentensi. Mfano enpi badala ya peni. Jina lingine huitwa sarufi maumbo.
b) **Shadda** ni kiwango cha nguvu kinachotumika kutamka silabi moja kuliko nyingine. Hujulikana kama mkazo kwa jina lingine.
c) **Fonimu** ni tamshi katika neno ambalo likibadilishwa na tamshi jingine maana ya neno hilo hubadilika au hupotoka katika lugha hiyo kama sabuni na zabuni hapa fonimu zinazotofautisha ni s na z.
d) **Alofoni** ni umbo lingine au jingine la mofimu ileile. Kibada cha mofimu kinachotokea kutokana na mazingira ya kiisimu bila kubadilisha maana.
e) **Shina** ni mzizi wa neno pamoja na kiambishi tamati maana. Mfano pik-a **(Alama 9)**

5. (a)
i) Mama amepika wali, nyama, maharage na ndizi
ii) Tanzania ilipata Uhuru mnamo Mwaka (1961)
iii) Mama Samia alisema “Kila mwananchi ni haki yake kupiga kura”
iv) Naomba niletee vifaa vifuatavyo: vya simu, redio na televisheni
(b)

i) Anaekutendea mabaya au anaekufanyia ubaya yu karibu na wewe

ii) Ukitaka kitu ni lazima ugharamike ama ukigharamikie

iii) Baada ya mateso na dhiki ni faraja.

**(Alama 9)**

6. Kutolea elimu
ii) Vyombo vya habari
iii) Biashara
iv) Kueneza dini (Kiislamu na Kikristo) **(Alama 9)**

7. Mtahiniwa anatakiwa kufuata taratibu za uandishi wa barua rasmi**(Alama 9)**

8. (a) Uchaguzi mkuu
(b) Miaka mitano
iii) Awe ammejiandikisha katika daftari la wapiga kura
awe na umri wa miaka kumi na nae n a kuendelea
Awe raia wa Tanzania na akili timamu
iv) Hutupatia viongozi bora

Huendeleza demokrasia
Huleta mabadiliko nchini na kutatua migogoro**(Alama 9)**
9. Utangulizi, mwanafunzi afafanue vizuri neno kuu la swali pia atambulishe Vitabu atakavyotumia na waandishi wake pia. **(Alama 15)**
**Utangulizi (Alama 2)**
**Kiini (Alama 12)**
**Hitimisho (Alama 3)**

**WASAKATONGE**
Kupiga vita uongozi mbaya "madikteta "unyama"
Kupiga vita ukoloni mambo leo "klabu""hatuna akili"
Kupiga vita matabaka "mvuja jasho" 'walala hoi"
Kuwa na demokrasia ya kweli na utu "Saddam Hussein""Madikteta"

**MASHAIRI YA CHEKACHEKA**
Kutetea haki "mwinyi umewasha moto"
Kupiga vita rushwa na ulanguzi "Mwinyi umewasha moto"
Kupiga vita ufuaji wa mali za umma "Gauni la mikutano"

**MALENGA WAPYA**
Kupiga vita matabaka "Samaki mtunoni "Punda"
Kupiga vita uongozi mbaya "Puuzo"bahari: n.k
Umuhimu wa kutumia pesa vizuri "Israfu"

**Hitimisho**: Mwanafunzi anatakiwa ahitimishe kulingana na swali lilivyoulizwa.

10. Utangulizi maana ya Fasihi (alama 02)
**Utangulizi (Alama 2)**
**Kiini (Alama 12)**
**Hitimisho (Alama 3)**

**TAADINI**
Kuacha mila potofu
Madhara ya vita
Uvumulivu
Ujasiri
Kukarimu wageni

**WATOTO WA MAMA NTILIE**
Kuepuka ulevi
Kushirikiana katika malezi ya baba na mama
Kuepuka vitendo viovu mfano wizi pamoja na madawa ya kulevya

11.
**Utangulizi (Alama 2)**
**Kiini (Alama 12)**
**Hitimisho (Alama 3)**

**NGOSWE PENZI KITOVU CHA UZEMBE**
Matumizi ya Tashbiha "He kwanza tazama sarawili yae miguuni kama Kengele ya bomani"
Tashbiha hii inamaanisha kuwa utamaduni wa watu wa vijijini na watu wa mjini ni tofauti.

Matumizi ya Midaa Midaa uliyotumiwa ni"Jama! Jama!" (uk 7) midaa hii inamaanisha kuwa tunatakiwa kujali katika swala la kuhesabu watu na hivyo kuwa tayari kuhesabiwa.

Matumizi ya Mdokezo, moja wapo ya mdokezo uliyotumiwa na mandishi ni "Sijui....... siwezi"napatikana uk 22. Mdokezo huu unamaanisha kuwa wasichana hawana msimamo maalumu wanaposhawishiwa na wanaume kwa kuwataka kimapenzi.

**KILIO CHETU**
Matumizi ya Tashibiha "Wakapukutika kama majani ya kiangazi" tamathali hii ya semi inamaanisha kuwa mazingira ya maisha hubadilika yatupasa kuishi ka tahadhari.

Matumizi ya Takriri "Vifo vikawazoa, vikawazoa" takriri hii inatupa tahadhari kuwa ugonjwa wa ukimwi nii hatari sana tunatakiwa kuwa makini na gonjwa hilo..

Matumizi ya Mdokezo "Joti..." mdokezo huu ulitolea na baba yake Joti huku akishangaa kuwa mwanae katika umri mdogo anaweza kuugua ugonjwa wa UKIMWI.